

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULIZA LEO**

**MKUTANO WA SABA**

**KIKAO CHA KUMI**

**20 APRILI, 2017**



# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA KUMI – TAREHE 20 APRILI, 2017

I. DUA:

II. KIAPO CHA UAMINIFU:

Mhe. Dkt. Getrude Pangalile Rwakatare.

III. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:

IV. MASWALI YA KAWAIDA:

WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:

80. MHESHIMIWA COSATO DAVID CHUMI (MAFINGA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:- Serikali katika mwaka 2016 imeeleza wazi kuwa haina mpango wa kununua magari ya wagonjwa na kwamba jukumu la kununua magari hayo limeachiwa Halmashauri za Wilaya ambazo hazimudu kununua magari hayo hali inayowafanya

baadhi ya wahisani kujitolea kununua magari hayo:-

Je, ni lini Serikali italeta mapendekezo ya kubadilisha Sheria ya Kodi ili magari hayo yaingie kwenye jedwali la saba na hivyo kupata msamaha wa kodi ya Ongezeko la Thamani.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA MAFUNZO YA UFUNDI:**

**81. MHESHIMIWA MARY PIUS CHATANDA (KOROGWE MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi:- Serikali imekuwa ikitoa majibu juu ya upandishwaji wa madaraja na fedha za likizo kwa Walimu nchini, na katika Chuo cha Ualimu Korogwe kuna Walimu na Watumishi ambao wanadai kupandishwa vyeo na fedha za likizo:-

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapandisha daraja wale wanaostahili;
- (b) Je, ni lini Serikali italipa madai yao ya fedha za likizo ambazo hawajawahi kulipwa.

## **WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:**

### **82. MHESHIMIWA OMARY TEBWETA MGUMBA (MOROGORO KUSINI MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Mto Ruvu ndiyo chanzo kikuu cha maji katika Mkoa wa Dar es Salaam:-

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kutenga fedha za kutunza mazingira katika vyanzo vya maji ambavyo viko katika hatari ya kukauka kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa na shughuli za kibinadamu;
- (b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwashirikisha wataalamu wa SUA katika utunzaji wa mazingira katika vyanzo vya maji katika Mkoa wa Morogoro.

### **83. MHESHIMIWA MARY DEO MURO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:-Maji ni mahitaji muhimu kwa wanadamu na viumbe vyote, lakini gharama za maji ni kubwa sana:-

Je, ni lini Serikali itawasambazia maji Wananchi waishio pembezoni mwa bomba kuu la Ruvu Juu Mlandizi – DSM katika maeneo ya Pangani, Lumumba, Kidimu na Zogowale ikizingatiwa kuwa maeneo hayo yapo karibu na bomba hilo.

## **WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:**

### **84. MHESHIMIWA RAISA ABDALLAH MUSSA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki:- Ofisi za Balozi za Tanzania hazipo katika hali nzuri na hii inatokana na ukosefu wa upatikanaji wa fedha ambazo zingeweza kuimarisha Balozi hizi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha tatizo hili linapatiwa ufumbuzi wa haraka ili kuendana na maendeleo ya dunia.

### **V. HOJA ZA SERIKALI:**

#### **WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (TAMISEMI, UTUMISHI NA UTAWALA BORA):**

Kwamba, Bunge likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais (TAMISEMI, Utumishi na Utawala Bora) kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

*(Majadiliano yanaendelea)*

**DODOMA  
20 APRILI, 2017**

**DKT. T. D. KASHILILAH  
KATIBU WA BUNGE**